

Sera ya Usimamizi wa mgeni Karatasi ya ukweli kwa Mpangaji

Idara ya Nyumba ina Sera ya Usimamizi wa Mgeni kusaidia wapangaji kusimamia wageni wao

Naweza kuomba namna gani ili mgeni akae?

Wageni wanaweza kukaa hadi wiki mbili (siku 14) kwa idhini yako. Kama mgeni wako anakwenda kukaa kwa muda wa zaidi ya wiki mbili ni lazima kuomba Idara ya Makazi ili kupata ruhusa.

Naweza kuomba namna gani ili mgeni akae?

Unahitaji kujaza Fomu ya Mgeni ya Kukaa Mda Zaidi, ili utwambia ni nani anayekaa nawe na kwa mda gani atakaa na wewe.

The Fomu inapatikana kutoka Ofisi ya Makazi ya karibu yako, na kwenye tovuti ya Idara ya Nyumba. Idara itatathmini maombi yako na kukupa taarifa ya matokeo. Tembelea ofisi ya makazi ya eneo lako kama unahitaji msaada kujaza fomu.

Ni wageni wangapi wanaweza kukaa na mimi kwa mda mmoja ?

Hii itategemea na idadi ya watu tayari wanaoishi na wewe, na idadi ya vyumba vilivyoko katika nyumba yako.

Naweza kupata msaada gani ili kutunza wageni wangu?

Kama unahitaji msaada kusimamia wageni wako, unaweza kupiga 131 444 au wasiliana na Ofisi ya Makazi yako ya mitaa au pigia Afisa wako wa Usalama wa Makazi wa Umma kwa 1800 685 743.

Rejea kwenye ukurasa 2 ili kupata mawasiliano na mahali pa ofisi za Idara ya Makazi.

Idara inaweza pia kukusaidia kusimamia wageni wako. Hii inaweza kujumuisha Idara kuzungumza moja kwa moja na wageni wako, kutoa barua kuomba wageni kuondoka, kutathmini idadi ya watu katika nyumba yako na kuamua kama watu wanakuwa wengi, au kukupa msaada kuititia Mpango wa Ustahili kwa Wapangaji

Kwa nini kuna kiwango maalumu cha wageni kukaa mahali?

Kama mpangaji wa Idara ya Nyumba, una wajibu kuhusiana na tabia ya wageni wako.

Kusimamia wageni husaidia kudumisha mahusiano mazuri na jamii na familia yako; kufurahia mazingira ya amani katika nyumba yako na majirani; na kuhakikisha nyumba yako haina msongamano mkubwa.

Je maombi yangu yatakubalika ?

Wafanyakazi wa idara wana haki ya kufikiria maombi kwa ajili ya wageni wanaokaa kwa muda mrefu zaidi ya wiki mbili (siku 14). Idara inaelewa kwamba wakati mwingine wageni wanahitaji kukaa muda mrefu kwa ajili ya utamaduni, michezo, sababu za matibabu au familia.

Idara itakataa wageni wa muda mrefu kama uwepo wao utasababisha msongamano, hawawezi kutoa ushahidi wa kuwa makazi ya kudumu mahali pengine, wana madeni kwenye Idara, au wao ni

mpangaji wa zamani au kutambuliwa kama mkazi wa Idara ya Makazi ambao walinyangwanywa makazi yako na idara ndani ya miaka miwili.

Nini kinatokea kama wageni wangu wanasababisha msongamano au tabia mbaya?

Kama msongamano ni tatizo, Idara inaweza kuuliza wageni kuondoka. Kama wageni wakikataa kuondoka, Idara inaweza kutumia chaguzi za kisheria kutekeleza sera.

Kama wageni wanasababisha tabia mbaya, unaweza kuuliza wageni wako kuondoka, au piga 131 444 kwa ajili ya misaada, au pigia ofisi ya makazi yako ya mtaa au Ofisi ya Umma ya Makazi Usalama kwa 1800 685 743

Idara inaweza kutoa onyo kwa wapangaji ili kusimamisha tabia mbaya au kuchukua hatua za kisheria.

Taarifa ya mwelekeo inaweza kuelekeza mtu asishiriki, au kuacha kujishughulisha, katika tabia zisizofaa. Kama mtu si mpangaji wa eneo husika, onyo linaweza kujumuisha mwelekeo kuondoka wa kuondoka.

Kama una wageni ambao wanasababisha msongamano, Idara inaweza kuuliza wageni wako kuondoka au inaweza kutoa onyo la hatia na ushirikiano wenu na ridhaa.

Idara pia inaweza kutoa taarifa kwa kurekebisha kasoro za uvunjaji wa mkataba wa upangaji wako ambayo unaweza kisha kuonyesha wageni wako. Unaweza kutumia taarifa hii kwa kuwaambia wageni kwamba hawawezi kuendelea kukaa kwenye nyumba yako.

Je sera hii inawahu su pia wapangaji wanaoishi katika maeneo ya vijijini?

Ndiyo.

Sera inatumika kwa wapangaji wote wa makazi ya umma na wageni wa makazi ya umma katika Mkoa wa Kaskazini.

Mawasiliano na Sehemu za Ofisi za Idara ya Nyumba

Casuarina - Cascom Centre, Trower Road	simu: 08 8922 5542
Darwin - RCG Centre, 47 Mitchell Street	simu: 08 8999 8814
Palmerston - Highway House, Chung Wah Terrace	simu: 08 8999 4767
Alice Springs – Level 1, Alice Plaza, 36 Todd Mall	simu: 08 8951 5344
Tennant Creek - NT Government Centre, Peko Road	simu: 08 8962 4497
Katherine - NT Government Centre, First Street	simu: 08 8973 8536
Nhulunbuy - Shop 2 Arnhem House, Endeavour Square	simu: 08 8987 0533